

## **TAMKO LA MTANDAO WA ELIMU TANZANIA KULAANI KITENDO CHA KUHADAA UBORA WA ELIMU KILICHOFANYWA NA BAADHI YA SHULE ZA MSINGI HAPA NCHINI**

Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) unaoundwa na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yapatayo 181 ya Tanzania Bara yanayoshughulika na maswala ya Elimu. Mtandao umepokea kwa mshituko na masikitiko makubwa taarifa juu ya shule zilizofutiwa matokeo ya mitihani ya darasa la saba kama ilivyoelezwa na Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani Tanzania hapo tarehe 2/10/2018.

Mtandao unalaani na kupinga vikali kitendo cha watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia elimu bora kwa watoto kuwatumia kama chambo cha kujipatia sifa na umaarufu.

Kitendo kilichofanyika ni hujuma kubwa ya juhudzi za serikali na wadau wengine wote za kuinua kiwango cha elimu hapa nchini. Lakini pia ni hujuma dhidi ya juhudzi za serikali za kupambana na rushwa na wizi wa aina zote.

Ikumbukwe kuwa mtoto wa darasa la saba hana uwezo wa kupinga anachoelekezwa na viongozi au walimu wake hivyo huamini kila anachoambiwa afanye ni chema bila kujua madhara yake ya baadae. Ni dhahiri kuwa kitendo cha kufutiwa matokeo ya mitihani kimewaathiri watoto kisaikolojia na kihisia na hivyo kuwapotenza uwezo wao wa kujiamini katika kufanya mitihani mingine na safari yao ndefu ya kutimiza ndoto zao.

Uamuzi wa kuwafanya waurudie mtihani ni jambo jema, inaonyesha Dhahiri kwamba kuna nia ya kuwapa fursa watoto hao. Hata hivyo muda uliotolewa wa kurudia mitihani hiyo ni mdogo sana kuwawezesha watoto kujiaandaa na kujengwa kisaikolojia ili kuwa tayari kwa kufanya mitihani. Tunapendekeza kuwa angalau wapewe mwezi mmoja wa kujiaandaa na kujengwa kisaikolojia.

Mtandao unaipongeza sana Serikali kwa kuweza kubaini kitendo hiki cha hujuma na kuchukua hatua za awali. Ni matarajio yetu kuwa uchunguzi utakapokamilika wale wote waliohusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria na kinidhamu ili iwe fundisho kwa umma.

  
Bi Cathleen Sekwao

Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET)

